

HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHE. ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (MB) WAKATI WA UZINDUZI WA BODI MPYA YA PAROLE YA MKOA WA RUKWA NA KATAVI TAREHE 26 JUNI, 2015

Mwenyekiti wa Bodi ya Parole Bibi Aurelia Pandisha Kanyegele

Waheshimiwa Wajumbe wa Bodi ya Parole

Ndugu waandishi wa Habari

Mabibi na Mabwana

Asalam aleykum!!

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutukutanisha mahali hapa siku hii ya leo.

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwasafirisha salama Wajumbe mnaotoka nje ya Mkoa wetu, napenda kutumia fursa hii kuwakaribisheni “karibuni sana”

Aidha nachukua fursa hii kwa uzito wa pekee kwa Waratibu wa shughuli hii, Jeshi letu la Magereza kwa Heshima hii kubwa mliyonipatia kuwa mgeni rasmi katika shughuli muhimu kabisa ya uzinduzi wa Bodi mpya ya Parole. “Asanteni sana kwa heshima ya kunialika kuwa mgeni rasmi”

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Pia napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wajumbe wa kuteuliwa na Mhe. Waziri kwa ajili ya kuingia katika Bodi hii ya Parole. Uteuzi wenu ulizingatia vitu vingi kwa kuwa jukumu lenu ni nyeti kwa Mkoa na Nchi kwa ujumla,

Sifa zenu zilizingatiwa kwa kuwa katika kutekeleza jukumu hilo la kushughulika na Watu mbalimbali waliotiwa hatiani ambao baada ya kujirekebisha mnawapa fursa ya kurudi uraiani kwa masharti ya kuwa watii wa sheria bila shuruti (raia wema).

Wito wangu kwenu ninyi na Wajumbe wote ambao mnaingia kwa nafasi zenu, " ni vema kuwa kuzingatia maadili" katika mienendo yenu katika shughuli zenu binafsi na utekelezaji wa Majukumu ya Bodi ya Parole.

Malengo ya uanzishwaji wa Bodi ya Parole kama ambavyo yalielezwa katika Taarifa ya Mkoa, malengo hayo kwa upande wangu naita Umuhimu wa uwepo wa Bodi ya Parole:-

- Kupunguza msongamano Magerezani
- Kuishirikisha Jamii katika suala la urekebishaji wa Tabia kwa wale wote walikutwa na hatia
- Motisha kwa wafungwa waliobaki gerezani kuwa na tabia nzuri ili waweze kunufaika na mpango huo wa kupunguziwa vifungo na adhabu.

Bodi ya Parole ni muhimu nami nakubaliana na uwepo wake kwa kuwa ni chombo mojawapo kinachosaidia kupelekeaa wote waliokutwa na hatia na kuhumumiwa adhabu mbalimbali kupata “2nd chance” baada ya kujutia makosa yao na kuonesha dalili njema ya kutorudia makosa yao.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sintazungumzia na kulishukuru Jeshi la Magerza kwa kutekeleza majukumu hususani katika urekebishaji wa tabia za wale wote ambao wanakutwa na hatia. Serikali inatambua umuhimu wa Jeshi hili katika kutekeleza majukumu kwenye changamoto nyingi bila manung’uniko wala kukata tama “Hongereni sana” huo ndiyo uzalendo uliotukuka.

Napenda kuhitimisha Hotuba yangu kwa kuwapongeza Jeshi la Magereza kwa jinsi ambavyo mnakabiliana na changamoto mbalimali katika utendaji kazi wenu hususani changamoto ya rasilimali fedha.

Sote tu mashahidi na tunajua namna ambavyo Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake katika hali ya kujitegemea baada ya ufadhili kutoka kwa Wadau wa Maendeleo kuzidi kupungua. Hivyo ni kweli kabisa rasilimali fedha imekuwa ikichelewa kutoka. Hata hivyo nafarijika kusikia kuwa mmekuwa mkijitahidi katika kukabiliana na changamoto zilizombe yenu kupitia vyanzo vyenu

vya ndani (miradi ya Maduka) huo ni mfano mzuri wa kuigwa na Taasisi nyingine.

Naendelea kutoa wito tuzidi kushirikiana ili changamoto zinazojitokeza tuweze kuzikabili kwa pamoja.

Mshimiwa Mwenyekiti,

Nimefahamishwa kuwa Bodi nitakayoizindua leo ni bodi ya nne (4) tangu ilipoundwa mwaka 2002/2004. tangu kuanzishwa kwa Bodi hizi manufaa yameonekana.

Baada ya kusema hayo nipo tayari kuzindua Bodi yetu mpya ya Parole ili iweze kutimiza wajibu wa kisheria uliopo katika Sheria No. 25 ya Mwaka 1994 inayotoa fursa ya kuachiwa wafungwa wenye sifa kutumikia sehemu ya vifungo vyao nje ya magereza.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Eng. Stella Martin Manyanya (Mb)

MKUU WA MKOA WA RUKWA